




**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



## USIMAMIZI WA MALIASILI NA HIFADHI YA BAIONUAI TANZANIA

Tanzania imejaliwa kuwa na maliasili nyingi na imeweka kipaumbele katika kulinda usalama wa viumbe hai vyake kwa kuweka zaidi ya asilimia 32 ya eneo lake la ardhi kwenye uhifadhi. Lakini, Tanzania inabaki kuwa moja ya nchi masikini zaidi duniani, ikiwa na idadi kubwa ya masikini wanaishi vijijini. Inakadiriwa kuwa hadi asilimia 80 ya wakazi wa vijijini wa Tanzania hutegemea utumiaji wa maliasili ili kujikimu kimaisha, jambo ambalo linafanya usimamizi wa rasilimali hizi iwe kipaumbele cha msingi k ukuaji endelevu.

Bioanuwai, haswa wanyama wa porini kama twiga, tembo na simba, ni muhimu kwa uchumi wa taifa, kwani utalii wa wanyama pori unachangia takribani asilimia tisa ya pato la taifa la ndani na asilimia 25 ya mapato yake ya kigeni. Nchini Tanzania, ongezeko la idadi ya watu, usimamizi mbovu wa mazingira, upanuzi wa kilimo, na mabadiliko ya tabia nchi pia kwa pamoja vinatishia baionuwai na kutishia hali ya maisha ya vijijini.

Kwa kugundua kuwa vyanzo vya umaskini na uharibifu wa bioanuwai vinashabihiana, USAID inashirikiana na serikali pamoja na watu wa Tanzania kuboresha usimamizi wa mazingira na usimamizi wa ardhi, pamoja na kujenga uwezo wa nchi katika kupunguza biasara haramu ya wanyama pori. Mkakati huu unajumuisha kuunda na kutekeleza sera muhimu za mazingira za kitaifa pamoja na kusaidia mipango ya hifadhi ya jamii.

## CHANGAMOTO

### USIMAMIZI WA MALIASILI NA HIFADHI YA BAIONUAI KWA UJUMLA

### KIWANGO CHA UFADHILI

Dola za Marekani milioni 9  
katika Mwaka wa Fedha  
2019

### WASHIRIKI WAKUU

- Wizara ya Maliasili na Utalii
- Division of Wildlife
- Huduma ya Misitu
- Mbuga za Taifa za Tanzania
- Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania
- Halmashauri za Wilaya
- Wildlife Conservation Society
- Taasisi ya Jane Goodall
- RTI International
- The Nature Conservancy
- Wizara ya Marekani ya Mambo ya Ndani

### MAEneo

Maeneo tengefu yaliyopewa kipaumbele:

- Ukanda wa Maasai kaskazini mwa Tanzania
- Ukanda wa Gombe – Masito – Ugalla Tanzania Magharibi
- Ukanda wa Ruaha kusini mwa Tanzania

### MAWASILIANO

Yoel Kirschner  
[ykirschner@usaid.gov](mailto:ykirschner@usaid.gov)

### KWA MAWASILIANO ZAIDI

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)  
Facebook: USAIDTanzania  
Twitter: @USAIDTanzania

USAID inafuata njia endelevu ya usimamizi wa mazingira hasa mazingira muhimu, pamoja na shoroba katika maeneo ya hifadhi. Wakati sera zenye tija zipo katika sekta zinazohusiana na usimamizi wa maliasili, ila sera hizi zinadhoofishwa katika kiwango cha utekelezaji kutokana na takwimu duni, uchakataji, na utekelezaji - unaosababishwa na uwezo dhaifu wa taasisi katika ngazi za serikali kuu na serikali za mitaa. Mbinu za usimamizi wa maliasili mara nyingi sio endelevu na hazifai, na kulazimisha wanakijiji wa eneo hilo kutumia rasilimali zao hovsky ili kuishi. Mwishowe, ujangili wa wanyamapori pia umeenea na kuwa tishio kwa mazingira na katika utalii.

## MATOKEO

- Mabadiliko makubwa ya sera yaliyopatikana: Jitihada za ufadhili za USAID zimekuwa zikihuksika moja kwa moja kwa maendeleo makubwa ya sera kwa idhini ya Serikali ya Tanzania. Hii ni pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, kanuni za eneo la wanyamapori, Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani, na kanuni za shoroba za Wanyamapori.
- Muundo wa usimamizi umeandaliwa na kufadhiliwa: Miradi ya usimamizi wa maliasili imeunda uwezo katika Baraza la Usimamizi wa Mazingira la Kitaifa, Kitengo cha Msada wa Usimamizi wa Wanyamapori, Ofisi ya Makamu wa Rais-Sekretarieti ya Mikakati ya Ofisi, Muungano wa Usimamizi wa Maeneo ya Wanyamapori ya Jamii, na mashirika ya kijamii.
- Juhudi za uhifadhi wa mazingira zimefanikiwa: Mabadiliko ya sera yanayofadhiliwa na USAID yaliruhusu hekta milioni tisa za ardhi muhimu ya kibaolojia kuwekwa chini ya usimamizi bora katika uhifadhi, kilimo endelevu, na matumizi mengine ya ardhi kwa takribani ya kipindi cha miaka 15 iliyopita.
- Maisha yameboreshwa: Miradi ya kijamii ya uhifadhi na usimamizi wa wanyamapori inawapa nguvu wenyeji kusimamia maeneo muhimu ya mazingira, na jamii zilizoathirika zinapata zaidi ya dola milioni 6 kutoka kwa wawekezaji binafsi. Tangu mwaka 2010, zaidi ya watu 400,000 wamepokea ongezeko moja kwa moja la faida za kiuchumi kuitia usimamizi endelevu wa maliasili na uhifadhi.
- Uhalifu wa wanyamapori umepungua: Kwa kushirikiana na idara mbalimbali za Serikali ya Marekani, ufadhili wa USAID umetoa mafunzo na kuandaa vifaa kwa maskauti walio katika maeneo yenye hatari kubwa imechangia kupunguza kwa asilimia 50 ya ujangili wa tembo tangu 2015. Hii iliungwa mkono na mipango ya ngazi ya jamii kupunguza motisha ya kujihusisha na ujangili na shughuli zingine haramu.